

Tafsiri kwa Kiswahili: Utz Diegner

Katika shule ya msingi, tulifundishwa kuziandika herufi sambamba. Maneno yalikuwemo kitabuni, kama ufumbuzi, ilibidi tu kuyasoma. Kamusi ilikuwa na maneno yote yaliyaremeka ndani. Ilikuwa sehemu ya ulimwengu wa watu wazima, lakini nilihisi kwamba kwa namna fulani ilituzidi, kamusi zilikuwa na uwezo wa kuuzidi uwezo wa binadamu. Lolote lile ulilolisema, ikiwa halimo kitabuni, halikuwa na maana. Mradi tu lilipokuwa limeandikwa humo.

Kamusi yaweka maneno sambamba ambayo maishani hayapatikani pamoja kamwe. Kamusi ni pahala pa kukutana ambapo bahati yenyewe ni sheria, kama orodha ya majina katika kitabu cha mahudhurio. Kitabu cha mahudhurio pia ni kamusi, ambamo kila mmoja huandikwa jina lake, siku yake ya kuzaliwa, jina la baba na kazi yake. Wajua kwamba wazazi wangu ni wahandisi umeme, na mimi ni mwana wa wahandisi umeme, kwa hivyo nayajua mambo ya umeme. Hakuwa na waandishi darasani, mradi ingaliwezekana kulipima jambo hili. Alfabeti ilielekea kuwa haishindiki, kama mstari wa wanafunzi wanaojipanga kwa urefu wao katika darasa la michezo. Kwa namna yoyote ile, alfabeti ilielekea kuwepo nje ya wakati uliohisika. Zamu ya nani leo? Wakati wa kuzaliwa kwangu, nilikuwa neno tayari.

Katika kamusi, kila neno ni la lazima, moja peke yake halina maana, ni pamoja tu yana maana, kama katika orodha ya majina.

Mshikamano wa maneno waumba lugha, kama mshikamano uzaliwavyo darasani, yaweza kuwa zamu ya kila mmoja, na kila siku yaanza na kuomwa kwa majina. Wayasoma ili wajue kama tunakuwepo, kuanzia A mpaka Z, kuanzia ablak mpaka zsiráf, kuanzia dirisha mpaka twiga, kuanzia Almási mpaka Zsuppán, sisi sote.